**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFIS YA RAIS**

**Anuani ya Simu**:
"UTUMISHI
**Simu**: 2118531/4
**Fax** 2131365
**BaruaPepe**:
**permsec@estabs.go.tz**

Menejimenti ya Utumishi wa Umma,
S. L. P. 2483,
**DAR ES SALAAM.**

Unapojibu tafadhali taja:

Kumbukumbu Na: C/AC.56/221/01/C/62 18 Oktoba, 2006.

# WARAKA WA WATUMISHI WA UMMA NA. 2 WA MWAKA 2006 KUHUSU HUDUMA KWA WATUMISHI WA UMMA WANAOISHI NA VIRUSI VYA UKIMWI NA WENYE UKIMWI

## *1.0 Utangulizi:*

1.1 Serikali ilitangaza kuwa UKIMWI ni janga la Taifa tangu mwezi Desemba, 1999, na ikasisitizwa juu ya umuhimu wa Taifa zima hususan viongozi wa serikali, wanasiasa, viongozi wa dini, mashirika yasiyo ya kiserikali, viongozi katika jamii na wananchi kwa ujumla kuchukua hatua za dhati na za makusudi za kuliweka taifa katika hali ya vita dhidi ya UKIMWI. Kufuatia tangazo hili, mwaka 2003, serikali ilianzisha kasma kwenye bajeti yake kwa ajili ya kuendeleza mapambano dhidi ya UKIMWI na virusi vya UKIMWI miongoni mwa watumishi wake.

1.2 Mwaka 2005, utafiti ulifanyika kwa lengo la kutambua madhara yanayosababishwa na virusi vya UKIMWI na UKIMWI kwenye Utumishi wa Umma ambapo matokeo ya utafiti huo yalionesha kuwa, watumishi wengi wameathirika na vifo vingi vinatokana na UKIMWI.

1.3 Utafiti huu umebainisha kuwa UKIMWI unachangia kupotea kwa kiasi kikubwa cha nguvu kazi tuliyonayo na kuathiri utendaji kazi katika Utumishi wa Umma.

## 2.0 *Madhumuni ya Waraka:*

Madhumuni ya Waraka huu ni:-

(i) Kuweka utaratibu rasmi wa namna ya kutoa huduma kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI, na wenye UKIMWI ili wawe na afya njema ya kuwawezesha kutumia ujuzi na taaluma walizozipata kwa gharama kubwa kwa faida yao, familia zao pamoja na Taifa zima kwa kutoa huduma bora.

(ii) Kuwahamasisha watumishi wajitokeze kupima na kujua hali ya afya zao ili wote ambao bado hawajaambukizwa waendelee kuwa salama na watumishi ambao wanaishi na virusi vya UKIMWI wapatiwe huduma zinazostahili na kuzuia maambukizi mapya.

## 3.0 *Kuwatambua wanaoishi na virusi vya UKIMWI:*

3.1 Mtumishi wa umma anayeishi na virusi au mwenye UKIMWI ana haki ya ajira na hapaswi kunyanyapaliwa.

3.2 Kila mwajiri anatakiwa kuweka utaratibu wa utoaji ushauri nasaha kwa watumishi watakaojitokeza kupima afya zao na kugunduliwa kuwa wana UKIMWI au wanaishi na virusi vya UKIMWI ili hatimaye waweze kupatiwa huduma zitakazotolewa na Serikali.

3.3 Kila mwajiri anatakiwa kufuata utaratibu wa serikali, kuchagua hospitali ya kutoa huduma kwa wafanyakazi pamoja na kubuni utaratibu wa kuwahamasisha watumishi kujitokeza kupima afya zao.

3.4 Kila mwajiri atateua hospitali au kituo kitakachotoa huduma ya ushauri nasaha kwa watumishi, huduma ya upimaji na huduma ya lishe (Nutritional Supplement) kwa watumishi watakaojitokeza kupima na kubainika wana Virusi vya UKIMWI.

3.5 Aidha watumishi ambao wataonekana hawana virusi vya UKIMWI watapewa ushauri nasaha unaolenga kuwafanya waepukane na tabia na vitendo vinavyoweza kuwaambukiza virusi vya UKIMWI.

3.6 Katika utekelezaji wa utaratibu huu inasisitizwa kuondoa hofu au hisia za unyanyapaa kwa watakaogundulika kuwa wanaishi na virusi vya UKIMWI au wana UKIMWI.

## *4.0 Huduma zitakazotolewa kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI:*

### *4.1 Aina za Huduma.*

Huduma zitakazotolewa na serikali kwa watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wenye UKIMWI zitawalenga watumishi pamoja na idadi ya wanafamilia walioanishwa kwenye Kanuni za Kudumu za Utumishi wa Umma za mwaka 1994.

#### *4.1.1 Huduma ya kupima na ushauri*

Huduma ya kupima na ushauri ni haki ya kila mtumishi na itatolewa bure katika hospitali zilizochaguliwa na mwajiri. Kila mwajiri ahamasishe watumishi wake kupima na kupata ushauri kuhusu afya zao.

#### *4.1.2 Huduma ya dawa*:

Serikali imeweka na itaendelea kutekeleza utaratibu ambapo watumishi wote wanaoishi na virusi vya UKIMWI watapatiwa dawa za kupunguza makali ya virusi hivyo. Huduma ya dawa hizo itatolewa bure katika hospitali zilizochaguliwa na Mwajiri kwa mtumishi wa Umma aliyejitokeza baada ya kupimwa na kuthibitika kuwa anaishi na virusi vya UKIMWI.

#### *4.1.3 Huduma ya chakula cha Mlo kamili:*

Watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI wanahitajika kula mlo kamili kila siku ili kuboresha afya zao na kuongeza nguvu mwilini. Mlo kamili husaidia kuongeza nguvu mwilini na kumsaidia mgonjwa asipate magonjwa nyemelezi mara kwa mara. Mlo kamili, ni mlo wenye mchanganyiko wa vyakula kutoka kwenye makundi makuu ya vyakula vya Wanga, Protini na Vitamini.

Ingawa ni vema vyakula hivi vikaliwa katika hali ya uasili, pale ambapo hali ya mtumishi hairuhusu vyakula hivyo kutumika katika hali ya uasili, vitolewe vyakula katika mfumo wa "nutritional food supplements" Huduma hii itatolewa na mtoa huduma atakayeteuliwa na mwajiri kushughulikia watumishi wenye Virusi vya UKIMWI na UKIMWI kutoka katika Wizara, Idara na Wakala wa Serikali.

*4.1.3 Huduma ya Usafiri:*

Mwajiri atagharamia usafiri na posho kwa mtumishi anayesafiri kwenda hospitali kupata matibabu ya magonjwa nyemelezi, kupima kiwango cha CD4 na kupata dawa za kurefusha maisha (ARV), kwa taratibu zilizowekwa na serikali, kwenye Kifungu cha J.2(a)(vi) cha Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 1994.

*4.1.4 Kazi nyepesi ( light duties )*

Waajiri wanashauriwa kuwapangia kazi nyepesi watumishi wanaoishi na virusi vya UKIMWI ili kuwawezesha kuendelea kutoa huduma katika sehemu zao za kazi. Kwa kazi za kitaalam watumishi wapunguziwe uzito wa kazi.

*Mwisho*:

**5.0** Inategemewa kuwa utekelezaji wa Waraka huu utapunguza athari za ongezeko la UKIMWI katika Utumishi wa Umma. Waajiri na watumishi wote wa Umma wanatakiwa kushiriki kikamilifu kupambana na UKIMWI.

**6.0** Waraka huu unaanza kutumika tarehe 1 Novemba, 2006.

Ruth H Mollel

<u>KATIBU MKUU ( UTUMISHI )</u>